

## NYIMBO ZA TAIFA NA JUMUIYA NA UTAMBULISHO WA JAMII

*Method Samwel*

*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Tanzania*

[methodsamwel16@gmail.com](mailto:methodsamwel16@gmail.com)

### **Ikisiri**

Wataalamu wa fasihi, utamaduni, muziki, anthrolopolojia na siasa wamekuwa wakizitazama nyimbo za taifa na jumuiya kama alama za utaifa na ujumuiya. Huzitazama kama nyenzo za kueleza tamaduni za taifa na jumuiya husika na kuleta umoja. Pia, huzitazama kuwa ni utambulisho wa taifa au jumuiya husika. Hata hivyo, uhakiki wetu wa nyimbo za Kiswahili za taifa na jumuiya umebainisha kuwa mtazamo huo una walakini. Hivyo, makala hii inabainisha maeneo mbalimbali yenye dosari katika wimbo wa taifa wa Tanzania, Kenya na wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Inaonesha kuwa dosari hizo zinazifanya nyimbo husika kushindwa kuwa utambulisho wa kweli wa taifa na jumuiya husika. Ili kubainisha hayo, makala hii inatumia Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii ya Tajfel na Turner. Aidha, makala hii inatokana na utafiti wa kitaamuli uliohusisha ushuhudiaji, mahojiano na udurusu na uchambuzi matini.

### **1.0 Utangulizi**

Nyimbo za taifa ni zile zilizoidhinishwa au kukubaliwa kutumika kama nyimbo rasmi za taifa husika na utambulisho unaowahimiza raia wake kuthamini taifa lao na kuhakikisha linakuwa salama (Cerulo, 1993; Bristowna Reed, 2002). Nyimbo hizo hutazamwa kama alama ya taifa husika na nyenzo muhimu ya kujenga uzalendo. Kwa kawaida, nyimbo hizo huimbwa katika matukio ya kitaifa kama vile sherehe za kumbukumbu ya uhuru wa taifa, uapisho wa viongozi wa kitaifa, wakati kiongozi mkuu wa taifa anapotaka kuhutubia taifa na katika maadhimisho mbalimbali ya kitaifa. Vilevile, nyimbo hizo huimbwa katika shughuli na maeneo kama vile taasisi za elimu, michezo ya kimataifa na shughuli nyinginezo muhimu (Kolsto, 2006; Gilboa na Bodner, 2009).

Nazo nyimbo za jumuiya ni zile zilizoidhinishwa au kukubaliwa kutumika kama nyimbo rasmi za jumuiya inayohusika. Nyimbo hizo hutambulisha jumuiya husika na kuonesha umoja na mshikamano wa wanajumuiya. Nyimbo za jumuiya huimbwa katika matukio yanayofanana na yale ambayo nyimbo za taifa huimbwa na mengine yenye umuhimu kijumuiya. Aidha, wimbo wa jumuiya huimbwa mara baada ya kumaliza kuimbwa wimbo wa taifa. Katika makala hii, tumehakiki nyimbo za Kiswahili za taifa la Tanzania, Kenya na wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Historia ya wimbo wa taifa wa Tanzania inasimuliwa kwa kina na Bornman (2006) na Sanga (2018). Sanga anaeleza kuwa wimbo huo ultangazwa rasmi mwaka 1961 kuwa wimbo wa taifa wa Tanganyika huru. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, wimbo huo uliboreshw na kuwa wimbo wa taifa wa Tanzania. Wimbo huo, unatokana na wimbo uliotungwa mwaka 1897, kwa lugha ya Kiksosa, uitwao *Nkosi Sikelel' iAfrika* (Mungu Ibariki Afrika). Wimbo huo wa Kiksosa ulitungwa na Enoch Mankayi Sontonga, aliyekuwa mfanyakazi katika shule ya misheni huko Afrika ya Kusini. Sontonga aliutunga wimbo huo ili uwe wimbo wa sala wa shule hiyo (Bornman, 2006; Sanga, 2018).

Hadi kifo cha Sontonga mwaka 1905, wimbo huo ulikuwa ukiimbwa kama wimbo wa sala katika shule aliyofundisha (Bornman, 2006). Hata hivyo, kama anavyofafanua Sanga (2018), mwaka 1912, wimbo huo ulifanywa kuwa wimbo wa sala wa chama cha siasa cha *African National Congress* (ANC) cha Afrika ya Kusini na mwaka 1925 ulifanywa kuwa wimbo rasmi wa ANC. Wimbo huo ultumika kufungulia na kufungia mikutano ya ANC. Mwaka 1927, Samuel Mqhayi, mshairi wa Kiksosa, aliongeza beti zingine saba katika wimbo wa Sontonga na wimbo huo ukaanza kusambaa Afrika. Baadhi ya beti za wimbo huo zenye mchanganyiko wa mashairi ya Sontonga (ubeti wa kwanza na kiti) na Mqhayi (beti zingine) unawasilishwa katika data (1):  
(1).

<b>Ubeti wa 1</b>	<b>Ubeti wa 1</b>
<i>Nkosi, sikelel' iAfrika</i>	<i>Mungu ibariki Afrika</i>
<i>Malupakam' upondo lwayo</i>	<i>Pembe yake iinuke</i>
<i>Yiva imitandazo yetu</i>	<i>Usikie maombi yetu</i>
<i>Uwazikelele</i>	<i>Na utubariki</i>
<b>Kiitikio:</b>	<b>Kiitikio:</b>
<i>Yihla Moya, yihla Moya</i>	<i>Shuka, eeh Roho</i>
<i>Yihla Moya Oyingcwele</i>	<i>Shuka, eeh Roho Mtakatifu</i>
<b>Ubeti wa 2</b>	<b>Ubeti wa 2</b>
<i>Sikelela iNkosi zetu;</i>	<i>Wabariki machifu wetu</i>
<i>Zimkumbule umDali wazo;</i>	<i>Wamkumbuke Mungu wao</i>
<i>Zimoyike zezimhlouele,</i>	<i>Wamhofu na kumnyenyeka</i>
<i>Aziskelele.</i>	<i>Ili uwabariki</i>
<b>Ubeti wa 3</b>	<b>Ubeti wa 3</b>
<i>Sikelel' amadol' esizwe</i>	<i>Wabariki wanaume</i>
<i>Sikelela kwa nomlisela</i>	<i>Wabariki pia vijana</i>
<i>Ulitwal' ilizwe ngomonde</i>	<i>Ili watumike kwa uvumilivu</i>
<i>Uwusikilele</i>	<i>Na uwabariki</i>
<b>Ubeti wa 4</b>	<b>Ubeti wa 4</b>
<i>Sikelel' amakosikazi</i>	<i>Wabariki wake</i>
<i>Nawo onk'amanenekazi</i>	<i>Na wanawake</i>
<i>Pakamisa wonk'umtinjana</i>	<i>Wainue watoto wa kike wote</i>
<i>Uwusikilele.</i>	<i>Na uwabariki</i>

**Chanzo:** Jules-Rosette na Coplan (2004)

Kutokana na mabadiliko yaliyofanywa na Mqhayi na wengine katika wimbo wa *Nkosi Sikelel' iAfrika*, kukawa pia na mabadiliko katika wimbo uliotumiwa na ANC. Wimbo huo kama ulivyotumika na ANC kufikia miaka ya 1930 unawasilishwa katika data (2):

(2).

<i>God, bless Africa</i>	Mungu, Ibariki Afrika
<i>Bless its leaders</i>	Wabariki viongozi wake
<i>Wisdom, unity, and peace</i>	Hekima, umoja na amani
<i>These are our shields</i>	Hizi ni ngao zetu
<i>Africa and its people</i>	Afrika na watu wake
 <b>Chorus:</b> <i>Bless Africa, Bless Africa</i>	 <b>Kiitikio:</b> Ibariki Afrika, Ibariki Afrika
<i>Bless us, the children of Africa</i>	Tubariki, watoto wa Afrika

**Chanzo:** Safaris (2014)

Kinachoonekana ni kuwa ubeti wa kwanza wa wimbo wa taifa wa Tanzania umechukuliwa kama ulivyo kutoka katika wimbo wa ANC. Ubeti wa pili ni maboresho ya ubeti wa kwanza, ambapo neno Afrika lilibadilishwa na kuwekwa Tanzania. Pia, yakachukuliwa baadhi ya maneno katika wimbo asilia wa Sontonga ya kuwaombea baraka wake, waume na watoto.

Mbali na Tanzania, wimbo wa “Mungu Ibariki Afrika” umeboreshwa na kutumiwa kama wimbo wa taifa wa Zambia (1964), Zimbabwe (1980 ingawa ulibadilishwa na kutungwa mpya 1994), Namibia (1990 ingawa ulibadilishwa na kutungwa mpya 1991) na Afrika ya Kusini (1997). Hivyo, wimbo huu umekuwa kama nembo ya Bara la Afrika (Bornman, 2006; Mutamererwa, Chamisa na Chambwera, 2013).

Nao wimbo wa taifa wa Kenya uitwao “Ee Mungu Nguvu Yetu” uliasisiwa mwaka 1963 wakati wa uhuru wa Kenya. Wimbo huo ultokana na tume maalum iliyopewa kazi ya kutunga wimbo wa taifa wa Kenya. Tume hiyo ilitembelea maeneo mbalimbali ya Kenya kutafuta mahadhi ambayo yangefaa kutumika katika wimbo huo. Tume hiyo iliishia kuyapata mahadhi ya pembejezi za Kipokomo ya *Bee Mdundo Bee* ambayo ndiyo yametumika katika wimbo wa taifa wa Kenya (Gathogo, 2015; Ngaira, 2015).

Nao wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaelezwa kwa kina katika *East African Community* [EAC] (2017). EAC (2017) inaeleza kuwa viongozi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, marais Pierre Nkurunziza (Burundi), Jakaya Kikwete (Tanzania), Yoweri Museveni (Uganda), Mwai Kibaki (Kenya) na Waziri Mkuu wa Rwanda, Bernard Makuza, katika mikutano wa 12 wa wakuu wa nchi, uliofanyika Arusha, Tanzania, tarehe 3 Disemba 2010, waliidhinisha wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika EAC, yanabainishwa mashairi ya wimbo huo, mwongozo wa uimbaji na mapigo yake ya muziki na bendi. Inaelezwa kuwa wimbo huo uimbwe katika shughuli zenyе umuhimu katika jumuiya; uimbwe au upigwe kwa ala za muziki; na uimbwe kwa ukamilifu na taadhima na kila mtu akiwa amesimama. Shughuli ambapo wimbo huu unatakiwa kuimbwa ni pamoja na mikutano ya viongozi wa jumuiya, maadhimisho ya jumuiya, wakati mkuu wa nchi mwanachama anapohutubia Bunge la Jumuiya, katika ufunguzi wa mikutano ya Bunge la Jumuiya na mikutano wa mwaka wa sheria wa Mahakama ya Jumuiya. Pia, wimbo huo unapaswa kuimbwa katika matukio ya jumuiya kama vile makongamano, michezo, matukio ya kiutamaduni, maonesho na matukio mengine kama nchi mwanachama itakavyoona inafaa. Katika mikutano na maadhimisho ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, beti zote tatu zinapaswa kuimbwa au kupigwa kwa ala. Katika matukio ambayo mkuu wa nchi mwanachama atakapokuwa amehudhuria, beti mbili zitaimbwa au kupigwa na katika shughuli nyinginezo, ubeti mmoja utaimbwa au kupigwa (EAC, 2017).

Wataalamu wa fasihi, utamaduni, muziki, anthropolojia na siasa wamekuwa wakizitazama nyimbo za taifa na jumuiya kama alama za taifa na jumuiya husika, nyenzo za kuelezea tamaduni na kuleta umoja (Cerulo, 1993; Bristow na Reed, 2002; Kolsto, 2006; Gilboa na Bodner, 2009). Wataalamu hao wanazitazama nyimbo hizo kuwa ni utambulisho wa taifa na jumuiya husika. Hata hivyo, uhakiki wetu wa nyimbo teule umebainisha kuwa mtazamo kuwa nyimbo hizo zinawakilisha tamaduni na utambulisho wa taifa na jumuiya husika una walakini. Hivyo, makala hii inawasilisha maeneo mbalimbali yenye dosari katika nyimbo teule yanayozifanya kushindwa kuwa utambulisho wa kweli wa taifa au jumuiya husika.

## 2.0 Methodolojia na Nadharia

Makala hii ni matokeo ya utafiti wa kitaamuli uliotumia usampulishaji lengwa. Sampuli iliyotumika ilizingatia nyimbo husika kuwa na toleo rasmi lililo katika lugha ya Kiswahili. Data zilikusanywa kwa kutumia ushuhudiaji, mahojiano na udurusu na uchambuzi matini. Mtafiti alihudhuria shughuli mbalimbali ambapo nyimbo teule zilitarajiwa kuimbwa ili kushuhudia iwapo zitaimbwaa au la, zitaimbwaje na iwapo zinafahamika na kukubalika kuwa utambulisho wa wahusika. Pia, mtafiti alifanya mahojiano na wanajamii husika ili kupata maoni yao kuhusu masuala hayo. Katika udurusu na uchambuzi matini, nyimbo teule zilikusanywa na kuhakikiwa. Kilichofanyika ni kubainisha mashairi ya nyimbo teule na kuhakiki iwapo yanatambulisha imani, maslahi na tamaduni za makundijamii mbalimbali yaliyopo katika taifa au jumuiya husika. Aidha, matini zingine kuhusu makundijamii yaishiyo katika mataifa na jumuiya ambazo nyimbo zao zilihakikiwa yalidurusiwa.

Uchambuzi na ufasiri wa data zilizotumika katika makala hii vimeongozwa na Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii ya Tajfel na Turner (Tajfel na Turner, 1979 na 1986). Nadharia hii inabainisha hatua tatu za utambulisho wa kijamii ambazo ni kujainisha, kujibainisha na kujilinganisha (Tajfel na Turner, 1986). Katika kujainisha, inaelezwa kuwa wanajamii hujitazama sifa, tabia au hali zao na kujiweka katika kundijamii la watu wenye sifa, tabia na hali zinazofanana na walizonazo. Katika kujibainisha, inaelezwa kuwa, baada ya kujainisha, wanajamii huanza kuishi kulingana na kundijamii walilojiainisha. Kwa upande wa kujilinganisha, inaelezwa kuwa, baada ya kujainisha na kujibainisha, wanajamii huanza kujilinganisha na makundijamii mengine yaliyopo katika jamii ili kuona iwapo wanapewa haki sawa. Inahitimishwa kuwa iwapo kundijamii moja litabaini kuwa kundijamii lingine linapendelewa, huweza kusababisha misuguano na hata vita na mauaji (Tajfel na Turner, 1979).

Hivyo, wananadharia hawa wanaeleza kuwa jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa makundijamii mbalimbali yanazingatiwa katika masuala

yanayowahusu ili kuondoa uwezekano wa kundijamii mojawapo kujiona kutothaminiwa. Wazo la msingi la Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, iliyoanza kutumika katika saikolojia, ni kuwa watu katika jamii hupenda kutambuliwa kutokana na makundi yao na kuona makundijamii hayo yakithaminiwa na kuzingatiwa (Tajfel na Turner, 1979 na 1986). Hivyo, ni muhimu masuala mbalimbali ya kijamii, ikiwemo fasihi, kuyazingatia makundi hayo. Katika fasihi, nadharia hii inaazimwa na kutumika kwa mrengo kuwa kazi za fasihi zinapaswa kuzitambulisha jamii zinazohusika. Kazi za fasihi zisipoweza kutambulisha jamii hizo, zinaweza kusababisha kutokubalika na kупингва. Pia, zinaweza kusababisha mvutano baina ya wanajamii. Hivyo, katika makala hii, nadharia hii imetumika kufanya tathmini ya jinsi nyimbo teule zinavyotambulisha makundijamii yaliyopo katika taifa na jumuiya husika.

### **3.0 Matokeo ya Utafiti na Mjadala**

Matokeo na mjadala umejikita katika masuala ya msingi yaliyomakinikiwa katika makala haya kama yanavyodadavuliwa katika vipengele vidogovidogo sehemu inayofuata.

### **3.1 Je, Nyimbo za Taifa na Jumuiya ni Utambulisho wa Kweli wa Taifa na Jumuiya?**

Kumekuwa na mjadala kuhusu nyimbo za taifa na jumuiya kutazamwa kuwa utambulisho wa taifa au jumuiya, na hivyo, kuibua mvutano katika jamii. Kwa mfano, nchini Tanzania, mwaka 2007, uliibuka mvutano baina ya Wakristo wa dhehebu la Mashahidi wa Yehova na serikali kuhusu wimbo wa taifa wa Tanzania (Kapama, 2013; Kibakaya, 2013; *Daily News*, 2013). Kapama (2013) anafafanua kuwa, katika mvutano huo, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, katika Wilaya ya Mbozi, mkoani Mbeya, ambao ni Mashahidi wa Yehova, walikataa kuimba wimbo wa taifa kwa madai kuwa wimbo huo unakinzana na imani yao. Kutokana na hilo, wanafunzi wattano walifukuzwa shule na wengine 122 walipewa adhabu zingine. Shauri lilifunguliwa mahakamani kupinga adhabu hizo. Tarehe 2 Disemba 2010, Mahakama Kuu ilitoa hukumu iliyoshadidia adhabu hizo kuwa zilikuwa sahihi. Hata hivyo, wanafunzi hao walikata rufaa katika Mahakama ya Rufaa. Tarehe 12 Julai 2013, hukumu ya awali ilibatilishwa na Mahakama

ya Rufaa na kusema kuwa, katika sheria za Tanzania, haielezwi kuwa ni lazima kuimba wimbo wa taifa (Kapama, 2013; Kibakaya, 2013; *Daily News*, 2013). Mvutano huu ni ishara ya kuwa kuzitazama nyimbo za taifa na jumuiya kuwa utambulisho wa taifa na jumuiya husika kuna walakini.

Kwa ujumla, uhakiki wa nyimbo teule ulibainisha kuwa nyimbo hizo si utambulisho wa kweli wa taifa au jumuiya. Hii ni kwa sababu nyimbo teule zimebainika kuwa na dosari mbalimbali zinazozifanya kukosa sifa ya kuwa utambulisho wa kweli wa makundijamii yaliyopo katika taifa na jumuiya zinazohusika. Mionganoni mwa dosari hizo ni pamoja na udhaifu wa kisheria; utungaji; nia ya kutungwa kwake; lugha zilizotumika; muundo; na mahadhi, sauti na mapigo. Dosari nyingine zipo katika utambulisho wa jamii, shughuli za kiuchumi na tunu za taifa na jumuiya; na uimbaji na upigaji. Dosari hizo zinafafanuliwa kwa kina katika vipengele 3.1.1 hadi 3.1.8:

### **3.1.1 Udhafu wa Kisheria**

Nchi na jumuiya mbalimbali zina sheria, katiba au itifikasi zinazobainisha nembo na utambulisho wao. Hata hivyo, imebainika kuwa si nyimbo zote za taifa zinabainishwa na sheria. Pia, hata zile zinazobainishwa na sheria, kuna dosari katika sheria hizo. Kwa mfano, Tanzania ina Sheria ya Nembo za Taifa ya Mwaka 1971, ambayo ingawa inazitaja nembo za taifa, wimbo wa taifa hautajwi. Pia, wimbo wa taifa wa Tanzania hautajwi katika Katiba ya Tanzania. Hivyo, wakati wimbo huo unatazamwa kama nembo ya taifa na utambulisho wake, suala hilo halina nguvu kisheria (Kapama, 2013). Kwa sababu hiyo, wimbo huo hauna uhalali kisheria kwani hakuna sheria yoyote ya Tanzania inayoutaja kuwa utambulisho wa Watanzania au nembo ya taifa la Tanzania (Kapama, 2013; Kibakaya, 2013; *Daily News*, 2013).

Kwa upande wa wimbo wa taifa wa Kenya, wenyewe unabainishwa katika Ibara ya 9 (1) (b) ya Katiba ya Kenya ya Mwaka 2010. Pia, Kipengele 2A (4) cha Sheria ya Bendera ya Taifa, Nembo na Majina (Sura ya 99 ya Sheria za Kenya) kinaubainisha wimbo huo kama utambulisho wa taifa la Kenya na kuzuia matumizi mabaya ya wimbo huo (*National Council for Law Reporting* [NCLR], 2011). Nao wimbo wa Jumuiya ya Afrika unabainishwa

katika Kipengele cha Nne cha Sheria ya Nembo za Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ilivyorekebishwa mwaka 2011 kuwa utambulisho wa jumuiya. Wimbo wa taifa wa Kenya na wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ingawa zinatajwa na kulindwa na sheria, ulinzi huo unaonekana kupitiliza na kuwanyima wanajamii haki ya kuzimiliki nyimbo hizo na kuwa utambulisho wao. Kwa mfano, sheria ya Kenya inakataza mtu ye yote kuukosoa wimbo wa taifa na kuudhihaki kwa namna yoyote (NCLR, 2011). Dhihaka kwa wimbo huo ni kosa la kulipishwa faini au kifungo au vyote viwili. Sheria za namna hiyo zinazuia watu kutoa maoni yao ya wazi kutaka kurekebishwa kwa wimbo wa taifa ili uwe utambulisho wao. Hivyo, wakati ambapo ni muhimu kuwa na sheria, katiba na itifikasi zinazolinda nyimbo za taifa na jumuiya, ni muhimu kwa sheria, katiba na itifikasi hizo kutoa uhuru wa kukosoa na kupendekeza marekebisho katika nyimbo hizo.

### **3.1.2 Udhafu katika Mchakato wa Utungaji**

Kama ilivyokwishakuelezw, wimbo wa taifa wa Tanzania unatokana na wimbo wa sala wa shule uitwao *Nkosi Sikele' iAfrika* uliotungwa na Sontonga, Mksosa wa Afrika ya Kusini. Hivyo, wimbo huo unatokana na utungo wa mtu ambaye si Mtanzania. Kutokana na hilo, ingawa uliongezwa ubeti unaohusu Tanzania, wimbo huo ni wa kigeni usiotambulisha Utanzania bali Uafrika ya Kusini.

Wimbo wa taifa wa Kenya nao, upatikanaji wake ulihusisha tume maalumu iliyokuwa na Wakenya, Thomas Kalume, Peter Kibukosya na Washington Omondi; Mganda, George W. Senoga-Zake; na Mwingereza, Graham Hyslop (Olali, 2015; Ngaira, 2015). Wakati Senoga-Zake alikwenda Kenya kufundisha na kuasi idara ya muziki katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Olali (2015) anafafanua kuwa Hyslop alikwenda Kenya mwaka 1936 na kuanza kufanya tafiti na kutunga kazi mbalimbali za fasihi. Hyslop alifanya tafiti nyingi katika jamii ya Wapokomo, ambayo mahadhi ya pembejezi yake yalitumika katika wimbo wa taifa. Kama ilivyokuwa kwa wimbo wa taifa wa Tanzania, utungaji wa wimbo wa taifa wa Kenya nao ulihusisha wageni. Kama anavyofafanua Ngaira (2015), Hyslop alikuwa ndiye mtozi wa usanii katika tume hiyo na aliyetunga mashairi ya wimbo huo. Aidha,

Senoga-Zake anatajwa kuwa mtaalamu wa muziki aliyejikuwa na uzoefu kuliko wengine katika tume hiyo. Hivyo, wanatume wageni walikuwa ndiyo watu wa kutegemewa sana kuliko wazawa katika upatikanaji wa wimbo wa taifa wa Kenya. Hata kutumika kwa mahadhi ya pembejezi ya Kipokomo katika wimbo wa taifa wa Kenya ni matokeo ya ushawishi wa Hyslop aliyefanya tafiti nyingi katika jamii hiyo. Aidha, kama anavyofafanua mmoja wa waliokuwa kwenye tume, Washington Omundi, wimbo huo ulipatikana kutokana na tume kutembelea maeneo mbalimbali ya Pwani nchini Kenya ili kutafuta mahadhi ambayo wimbo huo ungeyatumia (Ngaira, 2015). Tume hiyo haikutembelea maeneo yote ya Kenya au uwakilishi wa maeneo hayo. Hivyo, uhalali wake katika kuwatambulisha Wakenya wote una walakini.

Vilevile, tume iliyoundwa kutunga wimbo huo haikuwa wakilishi. Kama ilivyoelezwa awali, tume hiyo ilikuwa na Thomas Kalume (Mshauri wa Muziki na Mwinjilisti), Peter Kibukosya (Msanii wa Muziki), Washington Omondi (Mhadhiri wa Muziki), George Senoga-Zake (Profesa wa Muziki) na Graham Hyslop (Mwanafasihi). Hivyo, tume hiyo ilikuwa na msanii, wataalamu wa muziki, mwinjilisti na mwanafasihi. Tume hiyo haikuwa na makundi mengine ya Wakenya kama vile watu wasio na dini, wasio wasomi, wakulima, wafugaji na wanasiasa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, suala hili huweza kusababisha wimbo huo kutokubalika kwa wale ambao hawakuhusishwa.

Nao wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unatokana na mashindano ya kutunga wimbo wa jumuiya yaliyofanyika kuanzia tarehe 26 – 27 Septemba 2005 huko Arusha, Tanzania. Katika mashindano hayo, Richard L. Khadambi wa Kenya, alishinda nafasi ya kwanza na kulipwa Dola za Kimarekani 3,000; John J. Mugango wa Tanzania, alikuwa wa pili na kulipwa Dola 2,000; na Joseph Wasswa wa Uganda, alikuwa wa tatu na kulipwa Dola 1,500. Baada ya mashindano hayo, kamati maalumu ya wataalamu iliundwa ili kuunganisha tungo za washindi hao kupata wimbo mmoja wenye mchanganyiko wa ladha kutoka katika nchi tatu wanachama zilizotoa washindi (*The Citizen*, 2018a na 2018b). Hivyo, wimbo wa

Jumuiya ya Afrika Mashariki ulitokana na mawazo ya watu watatu walioshinda na kamati ya wataalamu iliyounganisha tungo zao. Utungaji wa wimbo huo haukushirikisha jamii pana ya wanajumuiya. Pia, katika mashindano ya kupata wimbo huo, ingawa kulikuwa na kamati ya kutathmini nyimbo zilizowasilishwa na ambayo ilikuwa na wajumbe kutoka nchi wanachama, ni vigumu kusema kuwa kulikuwa na haki katika kupata washindi. Hivyo, ni jambo linalotarajiwa kuwa kila mjambe angetamani mshindi atoke katika nchi yake. Akithibitisha hili, Oluoch (2015) anaeleza kuwa bado kuna hali ya kila nchi mwanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutetea maslahi yake. Suala hili linathibitishwa pia na *The Citizen* (2018a) linalobainisha kuwa, wakati Kenya inataka iaminike kuwa mtunzi wa wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Mkenya, Richard Khadambi, Tanzania nayo inataka iaminike kuwa mtunzi ni Mtanzania, John Mugango. Hivyo, inashawishi kuamini kuwa kupatikana kwa mshindi katika mashindano ya kutunga wimbo huo, kuliathiriwa sana na matamanio ya kila nchi kutaka mtunzi atoke kwao. Hali hiyo inawezekana kuwa iliathiri pia toleo la mwisho la wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliotokana na timu ya wataalamu waliounganisha nyimbo za washindi watatu.

Vilevile, washindi watatu ambao nyimbo zao ziliunganishwa hawakuwasilisha nyimbo zinazotambulisha nchi zao. Walitunga nyimbo hizo kwa utashi na maoni yao bila kuzingatia utambulisho wa nchi zao. Kwa hiyo, wanajumuiya kwa mapana yake, hawatambulishwi na wimbo uliopatikana. Pia, kwa kuwa wimbo ulioidhinishwa ulitokana na washindi watatu waliotoka Kenya, Tanzania na Uganda, hakuna utambulisho wa nchi nyingine wanachama kama vile Burundi, Rwanda na Sudani ya Kusini. Kama inavyoiezwa na wafuasi wa Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, suala hilo huweza kuufanya wimbo huo kutokubalika miongoni mwa wanajumuiya. Katika mahojiano tuliyoyafanya, wanajamii wengi katika nchi wanachama walikiri kutoujua wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wapo baadhi ya wanajumuiya ambao hawakuwa wanajua kuwa kuna wimbo huo na kuna wengine wanaojua kuwapo kwake lakini hawayajui mashairi yake. Ushuhudiaji ulibainisha kuwa hata baadhi ya viongozi katika

nchi zilizotafitiwa, hawayajui mashairi ya wimbo huo na hivyo ulipoimbwa kwenye shughuli wakiwepo, hawakuweza kuuimba.

### **3.1.3 Udhifu katika Nia ya Kutungwa na Aina ya Nyimbo**

Nia ya kutungwa kwa nyimbo za taifa na jumuiya na aina yenewe ya nyimbo ni eneo lingine lenye udhaifu. Baadhi ya nyimbo za taifa na jumuiya hazikutungwa kwa lengo la kuwa nyimbo za taifa au jumuiya. Kama ilivoyelezwa awali, wimbo wa taifa wa Tanzania ulipotungwa haukukusudiwa kuwa wimbo wa taifa bali wa sala. Hivyo, maudhui ya wimbo huo yanakosa utaifa bali yanaelekea kwenye udini. Kutokana na hilo, wimbo huo unakosa kuwa na uzito unaopaswa kuwapo katika wimbo ya taifa. Katika fasihi, nyimbo za dini (zikiwemo nyimbo za sala) zipo kundi tofauti na nyimbo za taifa na jumuiya (Ngure, 2003; Wamitila, 2010). Kwa mujibu wa wataalamu hao, nyimbo za dini zinahusu masuala ya kidhanifu na yasiyo na ithibati kisayansi na pia zinahusu Mungu na uwezo wake. Nyimbo za taifa au jumuiya, kwa upande wake, zinapaswa kuhusu masuala halisi yanayotambulisha taifa au jumuiya husika. Zinapaswa kutambulisha mambo halisi ya kiutamaduni, kisiasa, kijamii na kiuchumi ya taifa au jamii husika (Ngure, 2003; Wamitila, 2010). Hivyo, kuufanya wimbo uliotungwa kuwa wa sala kuwa wimbo wa taifa kumeufanya wimbo huo kushindwa kutambulisha makundijamii husika katika masuala mbalimbali ya kiuchumi-jamii.

Kwa upande wa wimbo wa taifa wa Kenya, ultungwa kwa nia ya kupata wimbo wa taifa. Hata hivyo, kuna walakini katika wimbo wenewe uliopatikana ambao umetokana na mahadhi ya pembejezi. Wimbo wa taifa wa Kenya kutokana na pembejezi ni udhaifu mkubwa. Hii ni kwa sababu pembejezi ni nyimbo za kubembelezea watoto na hazina sifa za utambulisho wa jamii zinazopaswa kuwapo katika wimbo wa taifa. Pia, pembejezi ni utanu wa fasihi simulizi ulio katika kundi la tumbuizo, yaani nyimbo zinazotumika kutoa burudani. Nyimbo za taifa na jumuiya, kwa upande mwingine, ni fasihi simulizi zilizo katika kundi la tukuzo, yaani nyimbo za kusifia au kutokuza (Ngure, 2003; Wamitila, 2010). Wimbo wa taifa au jumuiya unapoimbwa, unapaswa kuwa na nguvu ya kumfanya mtu kulia

akitambua wajibu mkubwa alionao kwa taifa au jumuiya yake (Gilboa na Bodner, 2009). Wimbo uliotungwa kama tumbuizo hauwezi kumfanya mtu kulia bali kumtumbuiza na kumpa starehe.

Nao wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ingawa ultungwa kwa nia ya kuwa wimbo wa jumuiya, nyimbo zilizoteuliwa na kuunganishwa ili kupata wimbo huo hazikutungwa ili ziwe nyimbo za jumuiya. Kwa mfano, wimbo uliowasilishwa na Mtanzania John Mugango unafanana sana na wimbo wa taifa wa Tanzania, ambao kimsingi ni wimbo uliotungwa kuwa wimbo wa sala. Kama ilivyoelezwa awali, wimbo wa sala hauwezi kuwa utambulisho wa masuala ya kiuchumi-jamii.

### **3.1.4 Udhafu katika Lugha Zilizotumika**

Mbali na dosari hizo, lugha zilizotumika katika nyimbo teule ni eneo jingine lenye udhaifu. Wimbo wa taifa wa Tanzania unatumia lugha ya Kiswahili. Ingawa inakubalika kuwa lugha hii ndiyo iliyoenea zaidi Tanzania, ni ukweli usiopingika kuwa Tanzania ina lugha za makabila zaidi ya 158 (Msanjila, 2003; Gahnström, 2012). Kuna makabila ambayo hayazungumzi wala kuelewa Kiswahili. Pia, kuna wanajamii ambao umahiri wao katika lugha hiyo ni mdogo na wasingependa kutambulishwa kuwa ni watumiaji wa Kiswahili. Wanajamii hao huweza kuwasiliana vizuri zaidi kwa kutumia lugha zao za makabila kuliko Kiswahili. Kimsingi, wanajamii hao hawauelewi wimbo wa taifa wa Tanzania wala maana yake. Kwa mfano, wakati wa utafiti huu katika Kijiji cha Misuma wilayani Masasi, nchini Tanzania, tuliwashuhudia wanajamii wengi wasiojua kabisa Kiswahili bali Kimakua. Hali kama hiyo tuliishuhudia wilayani Bukoba Vijijini na Lushoto nchini Tanzania. Bukoba Vijijini tulishuhudia watu wengi wakitumia zaidi Kihaya kuliko Kiswahili. Hata katika ofisi ya wilaya, tulishuhudia matangazo yanayowataka wafanyakazi na wageni kutumia Kiswahili badala ya Kihaya. Mahojiano yetu na wahuksika yalibainisha kuwa tangazo hilo liliwekwa kutokana na matumizi ya Kihaya kuwa makubwa katika ofisi hizo. Nako Lushoto tulishuhudia idadi kubwa ya wanafunzi wakitumia zaidi Kisambaa kuliko Kiswahili. Hata wakati wa kufundisha, tulishuhudia walimu wakitumia Kisambaa kufafanua dhana ambazo zilishindwa kueleweka katika Kiswahili. Mahojiano yetu na walimu hao

yalibainisha kuwa wanafanya hivyo kwa kuwa Kiswahili hakieleweki vizuri kwa wanafunzi hao. Hii ni ithibati kuwa kuna Watanzania ambao umahiri wao katika lugha ya Kiswahili ni mdogo. Pia, inabainisha kuwa kuna Watanzania ambao wasingependa kutambulishwa kuwa watumiaji wa Kiswahili bali wa lugha zao za makabila. Kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, kuzilamisha jamii hizo kuutazama wimbo wa taifa wa Tanzania wa Kiswahili kama utambulisho wao kunaweza kusababisha misuguano na kutokubalika kwa wimbo huo.

Hali kama hiyo, inaonekana nchini Kenya ambapo mashairi asilia ya wimbo wa taifa yalitungwa kwa Kiswahili. Baadaye, mashairi hayo yakatafsiriwa katika Kiingereza na kuufanya wimbo huo kuweza kuimbwa katika lugha mbili. Hata hivyo, Kenya ina makabila zaidi ya 40 (Lenjima, 2019). Kama ilivyo Tanzania, kuna makabila nchini Kenya ambayo yana idadi kubwa ya watu ambao hawana umahiri katika Kiswahili wala Kiingereza. Hivyo, matumizi ya lugha hizo katika wimbo wa taifa yanaufanya wimbo huo kukosa sifa ya kuwa utambulisho wao. Pia, Kiingereza si lugha yenye asili yake nchini Kenya na si mojawapo ya lugha za Kiafrika. Hivyo, matumizi yake katika wimbo wa taifa yanaufanya wimbo huo kushindwa kuwa utambulisho wa Wakenya. Kwa kuwa wimbo wa taifa ni utambulisho wa taifa husika, lugha inayotumika inapaswa kuwa na asili katika taifa hilo. Aidha, lugha hiyo inapaswa kuwa utambulisho wa makundijamii yaliyopo katika nchi hiyo. Mfano wa hili tunaupata Zimbabwe ambapo, baada ya uhuru mwaka 1980, walikuwa na wimbo wa taifa ulioitwa kwa Kishona *Ishe Komborera Africa/Zimbabwe* (Mungu Ibariki Afrika/Zimbabwe), na ambao ulikuwa na mashairi ya Kishona na Kindebele. Wimbo huo ultokana na wimbo wa *Nkosi Sikelel' iAfrika* (Vambe na Khan, 2009; Mutamererwa na wenzake, 2013). Hata hivyo, Wazimbabwe waliona kuwa wimbo huo hauna asili ya Zimbabwe wala hauwatambulishi wao bali Waafrika Kusini. Pia, wimbo huo ulionekana kuwa katika lugha mbili tu wakati Zimbabwwe hutumia lugha nyingi zaidi. Kutokana na hayo, wimbo huo ulibadilishwa mwaka 1994 na kutungwa mpya uitwao *Simudzai Mureza wedu WeZimbabwe* (Inua Juu Sana Bendera Yetu ya Zimbabwe) ambao pia unaitwa kwa Kindebele "*Kalibusiswe Ilizwe leZimbabwe*" (Mutamererwa na

wenzake, 2013; Ndimandea na Moyo, 2018). Kwa kuwa Zimbabwe ina jamiilugha mbalimbali, wimbo huu upo katika lugha hizo zinazojumuisha Kishona, Kindebele, Kiingereza, Kisotho, Kiswana, Kichewa, Kibarwe, Kikalanga, Kikoisani, Kinambya, Kimbau, Kishangani, Kitonga, Kivenda na Kiksosa (Vambe na Khan, 2009; Mutamererwa na wenzake, 2013; Ndimandea na Moyo, 2018). Hali kama hiyo inaonekana katika wimbo wa taifa wa Zambia ambao upo katika lugha nne: Kibemba, Kichewa, Kitonga na Kiingereza (Wakumelo, 2013). Hata hivyo, suala la wimbo wa taifa au jumuiya kutambulisha jamiilugha zote zilizopo katika taifa au jumuiya husika ni rahisi kutekelezwa kama jamiilugha hizo si nyingi. Suala la msingi ni kuwa hata pale wimbo wa taifa au jumuiya unaposhindikana kuwa katika lugha zote zilizopo, itumike lugha ambayo kwa namna fulani itatambulisha jamiilugha zilizopo katika taifa au jumuiya hiyo.

Kwa upande wa wimbo wa Afrika Mashariki, wenyewe upo katika lugha ya Kiswahili. Ingawa Kiswahili ni lugha rasmi ya jumuiya, matumizi ya lugha hiyo katika wimbo wa jumuiya yana walakini. Kwanza, japokuwa Kiswahili kinafaa kuwa lugha rasmi ya kuitambulisha Afrika, matumizi yake katika wimbo huo hayakuhusisha mjadala mpana katika mataifa husika wala raia wa kawaida. Kwa kiasi kikubwa, yalikuwa majadiliano ya viongozi na vyombo mbalimbali. Pia, Kiswahili si lugha rasmi ya Sudani Kusini na matumizi yake nchini Rwanda ni madogo. Hivyo, matumizi yake katika wimbo wa jumuiya yanawafanya wakazi wengine kutouelewa na kutotambulishwa nao. Katika mahojiano tuliyoyafanya katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo matumizi ya Kiswahili ni madogo, watoa taarifa wengi walibainika kutoujua wimbo huo. Nchini Rwanda, kwa mfano, idadi kubwa ya watoa taarifa katika Wilaya ya Kicuciro jijini Kigali, hawakuweza kabisa kuuimba wimbo huo kutokana na kutojua kabisa Kiswahili. Hii ni kinyume na Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii inayotaka makundijamii yote kuzingatiwa katika kazi mbalimbali za fasihi zinazowahusu ili kuzifanya kazi hizo kukubalika.

Pia, suala la lugha ya kutumika katika wimbo wa taifa na jumuiya limebainika kuwa na changamoto kubwa pale ambapo wimbo husika upo

katika lugha mbili na tafsiri kutofanywa vema. Hilo huweza kusababisha mashairi katika lugha zilizotumika kupishana. Tatizo hili linabainika katika wimbo wa taifa wa Kenya ambapo mashairi ya Kiswahili na Kiingereza hayawasilishi dhana sawa.

(3).

<b>Mashairi ya Kiswahili</b>	<b>Tafsiri yake ya Kiingereza</b>	<b>Tafsiri sahihi ya Kiingereza</b>
1 Ee Mungu nguvu yetu Ilete baraka kwetu. Haki iwe ngao na mlinzi Na tukae na undugu... Raha tupate na ustawi	1 <i>O God of all creation Bless this our land and nation.</i> <i>Justice be our shield and defender</i> <i>May we dwell in unity...</i> <i>Plenty be found within our borders.</i>	1 <i>O God our strength Bring blessing to us</i> <i>Justice be a shield and defender</i> <i>And may we dwell in comradeship</i> <i>May we get pleasure and welfare</i>
2 Amkeni ndugu zetu Tufanye sote bidii Nasi tujitoe kwa nguvu Nchi yetu ya Kenya, Tunayoipenda Tuwe tayari kuilinda.	2 <i>Let one and all arise With hearts both strong and true.</i> <i>Service be our earnest endeavour,</i> <i>And our Homeland of Kenya</i> <i>Heritage of splendour,</i> <i>Firm may we stand to defend.</i>	2 <i>My comrades wake up</i> <i>We should perform with devotion</i> <i>And we should sacrifice ourselves</i> <i>Our country Kenya</i> <i>The way we love it</i> <i>We should be ready to defend</i>
3 Na tujenge taifa letu Ee, ndio wajibu wetu	3 <i>Let all with one accord</i> <i>In common bond united,</i>	3 <i>And we should build our nation</i>

Mashairi ya Kiswahili	Tafsiri yake ya Kiingereza	Tafsiri sahihi ya Kiingereza
Kenya istahili heshima	<i>Build this our nation together</i>	<i>O its our responsibility Kenya deserves respect</i>
Tuungane mikono	<i>And the glory of Kenya</i>	<i>Let us join our hands</i>
Pamoja kazini	<i>The fruit of our labour</i>	<i>Together in work</i>
Kila siku tuwe na shukrani.	<i>Fill every heart with thanksgiving</i>	<i>Everyday we should be thankful</i>
<b>Chanzo:</b> NCLR, 2011	<b>Chanzo:</b> NCLR, 2011	<b>Chanzo:</b> Tafsiri Yangu

Katika data (3), imebainika kuwa mistari karibu yote, isipokuwa miwili, ina tafsiri isiyio sahihi. Kutohana na hilo, tafsiri sahihi imebainishwa katika kolamu ya mwisho. Huu ni uthibitisho kuwa wanachokiiimba katika Kiingereza na Kiswahili ni tofauti kabisa. Suala hili linaibua swali kuwa, je, wimbo wa taifa wa Kenya, ambao ni utambulisho wa Wakenya ni ule ulio katika Kiswahili au Kiingereza?

### 3.1.5 Udmaifu katika Muundo na Mahadhi

Nyimbo teule za taifa na jumuiya zina udhaifu katika muundo na mahadhi yake. Nyimbo hizo zimeshindwa kutambulisha kwanza masuala ya kipaumbele kwa nchi na jumuiya na watu wake. Wimbo wa taifa wa Tanzania unaanza ubeti wa kwanza kwa dua kwa Afrika na kisha ubeti wa pili una dua kwa Tanzania kama inavyowasilishwa katika data (4): (4).

- |   |   |
|---|---|
| <p>(a) <b>Mungu Ibariki Afrika,</b><br/> <b>Wabariki Viongozi Wake,</b><br/>           Hekima, umoja na amani<br/>           Hizi ni ngao zetu<br/> <b>Afrika na Watu Wake</b> (ubt. 1)</p> | <p>(b) <b>Mungu Ibariki Tanzania,</b><br/> <b>Dumisha Uhuru na Umoja,</b><br/> <b>Wake kwa Waume na Watoto,</b><br/>           Mungu, Ibariki,<br/> <b>Tanzania na Watu Wake</b> (ubt. 2)</p> |
|---|---|

#### Kiitikio

Ibariki, Afrika,  
 Ibariki, Afrika,

#### Kiitikio

Ibariki, Tanzania,  
 Ibariki, Tanzania,

**Tubariki, Watoto wa Afrika,      Tubariki, Watoto wa Tanzania**

**Chanzo:** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania [JMT], ht.

Katika data (4), ikitumika kanuni ya lililo muhimu litajwe kwanza, kama inavyofafanuliwa na Nikitina (2011), wimbo huo unamaanisha kuwa, kwa Watanzania, Afrika ni bora kuliko Tanzania na wanapenda kutambuliwa kwa Uafrika wao kuliko Utanzania wao. Kwa hakika suala hili si sahihi. Kwa upande wa mahadhi, kama tulivyoeleza awali, wimbo huo unatumia mahadhi, mapigo na sauti asilia ya Kiksosa; mahadhi hayo yana asili ya Afrika ya Kusini. Wimbo wa taifa unapaswa kutumia mahadhi ya jamii za taifa husika ili kuwa utambulisho wao (Cerulo, 1993; Kolsto, 2006).

Kwa upande wa wimbo wa taifa wa Kenya, muundo, mahadhi, sauti na mapigo yake pia yamebainika kuwa na dosari. Kimuundo, wimbo huo unaanza kwa kumtaja Mungu kuwa nguvu za wananchi wa Kenya. Unaonesha kuwa Mungu ndiye ana jukumu la kuleta baraka ili Kenya iwe na haki, watu wakae kwa udugu na pia kuwe na amani, uhuru, raha na ustawi kama inavyobainishwa katika ubeti wa 1 katika data (3). Kwa kanuni ya la muhimu kusemwa kwanza (Nikitina, 2011), kwa Wakenya, kumtegemea Mungu kunaonekana kuwa suala la muhimu na ndio utambulisho wao kuliko kutumia juhudzi zao kufanya kazi kwa bidii. Dhana hii inakinzana na uyakinifu na haiwasilishi mawazo ya Wakenya wote. Katika majadiliano tuliyoyafanya na baadhi ya wakazi wa Kaunti ya Baringo nchini Kenya kuhusu nafasi ya Mungu katika maisha yao, wengi wao walituthibitishia kuwa juhudzi zao ndizo huweza kuwalettea ustawi na wala siyo Mungu.

Nao wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unatumia muundo unaofanana na wa Tanzania na Kenya. Unaanza kwa dua kwa Mungu ili ailinde Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuifanya iwe na amani na itimize malengo yake kama inavyobainishwa katika data (5):

(5).

**Ee Mungu twaomba uilinde**

Jumuiya Afrika Mashariki

Tuwezeshe kuishi kwa amani  
Tutimize na malengo yetu (ubt. 1)  
**Chanzo:** EAC, 2017

Kimsingi, ubeti huu ni wa kidhanifu na hautambulishi imani za wananchi wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Si wanajumuiya wote wanasubiri Mungu ailinde jumuiya badala ya wao kutumia juhudi zao. Hili lilithibitishwa na utafiti wetu wa uwandani katika Jiji la Bujumbura ambapo tuliweza kuwabaini watu kadhaa ambao hawaamini suala la Mungu kuwalinda watu.

Kuhusu mahadhi, wimbo huo una mahadhi mchanganyiko ya wimbo uliotungwa na Mkenya, Richard Khadambi, ambaye alikuwa mfanyakazi wa Benki Kuu ya Kenya na mwalimu wa kwaya katika kanisa la Pentekoste Nairobi, Kenya; Mtanzania, John Mugango, aliyekuwa mwalimu na msanii wa Bukoba; na Mganda, Joseph Wasswa, aliyekuwa mwanafunzi wa mwaka wa pili wa muziki katika Chuo Kikuu cha Makerere. Wimbo huo, kwa kiasi kikubwa, una mahadhi ya sala kutohana na watunzi wake kutamani kutunga wimbo unaofanana mwelekeo na nyimbo za mataifa yao. Hili linathibitika kwa John Mugango ambaye wimbo wake aliuита “Mungu Ibariki Jumuiya ya Afrika Mashariki,” akiufananisha na wimbo wa taifa wa Tanzania uitwao “Mungu Ibariki Tanzania.” Kama tulivyoeleza awali, matumizi ya mahadhi, sauti na mapigo ya sala katika wimbo wa taifa ni suala lenye walakini.

### **3.1.6 Udhaifu katika Utambulisho wa Jamii, Imani na Shughuli za Kiuchumi**

Vilevile, imebainika kuwa nyimbo teule zina udhaifu katika utambulisho wa jamii, imani za kidini na shughuli za kiuchumi. Wimbo wa taifa wa Tanzania hautambulishi kabisa shughuli za kiuchumi za Watanzania. Kuhusu utambulisho wa jamii, wimbo huo unayataja makundijamii kama vile viongozi na watu wa Afrika; watoto wa Afrika; wanawake, wanaume, watoto na watu wa Tanzania; na watoto wa Tanzania (taz. data 4 a na b). Hata hivyo, wimbo huu unawatambua watoto lakini hauyatambui makundi jamii mengine kama vile vijana na wazee. Hivyo, kuutazama wimbo huu

kama utambulisho wa Watanzania pamoja na mawazo na matamanio yao ni suala lenye walakini.

Kwa upande wa imani, wimbo wa taifa wa Tanzania unaonekana kuzingatia imani katika Mungu. Wimbo huo unaonesha kwamba taifa zima la Tanzania linaundwa na watu wanaoamini katika Mungu, suala ambalo si la kweli. Kama anavyosema Van Pelt (1971), Tanzania ina kundi kubwa la watu ambao hawaamini katika dini wala Mungu. Hivyo, kumtaja Mungu katika wimbo wa taifa ni suala linalowatenga watu hao. Pia, Ibara ya 9 (d) ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 inabainisha kuwa taifa la Tanzania litatoa haki sawa kwa raia wote bila kujali jinsi, dini, rangi, kabilia au hali ya mtu. Aidha, Ibara ya 19 (2) inabainisha kuwa shughuli za kidini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi (Mpiga Chapa wa Serikali, 2000). Hivyo, wimbo wa taifa kuingiza imani za dini na kuwazingatia wenye dini tu ni kwenda kinyume na katiba. Pia, kama wanavyoeleza wafuasi wa Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, kutowazingatia wasio na dini kunaufanya wimbo huo kutokuwa utambulisho wao.

Wimbo wa taifa wa Kenya, hauna tofauti kubwa na wa Tanzania. Kwa kuanza na kumhusisha Mungu na maendeleo ya Kenya kama ilivyonukuliwa katika data (3), kunamaanisha kuwa wimbo huo nao unawabagua wasio na dini. Suala hilo ni kinyume cha Katiba ya Kenya kwani Ibara ya 8 ya Katiba hiyo inabainisha kuwa nchi ya Kenya haina dini ya taifa. Hii ina maana kuwa masuala ya Mungu hayatambuliwi katika katiba hiyo (NCLR, 2013). Hata hivyo, wimbo huu, tofauti na wa Tanzania, ambao umewatambulisha Watanzania kama watu wanaomtegemea Mungu tu, unawatambulisha Wakenya kuwa wanafanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo na ustawi. Wimbo huo unawatambulisha Wakenya kama watu wanaojitoa kwa nguvu kuilinda nchi yao. Watunzi wa wimbo huu wamejitahidi kuwatambulisha Wakenya wenye dini na wasio na dini. Hata hivyo, ingawa wimbo huo umewatambulisha Wakenya kama watu wanaofanya kazi kwa bidii umezitaja kazi hizo kiujumla. Kutaja kazi kiujumla ni suala jema kwa kuwa si rahisi katika wimbo wenye beti chache kubainisha kazi zote zinazofanywa na wananchi wote. Hata hivyo, ni dhahiri

kuwa si kweli kuwa nchini Kenya watu wote wana kazi. Mahojiano yetu na wananchi jijini Nairobi yalibainisha kuwapo kwa kundi kubwa la vijana wasiokuwa na kazi.

Nao wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaonekana kuwa na walakini katika utambulisho wa jamii, imani za kidini na shughuli za kiuchumi. Wimbo huo, kama ulivyo wa Tanzania na wa Kenya, ni dua ya kumwomba Mungu ailinde jumuiya. Kama ilivyobainishwa awali, si wananchi wote wa Afrika Mashariki wanaamini katika Mungu. Tofauti na wimbo wa Tanzania, wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zaidi ya kubainisha kuwa wanajumuiya wanaamini kuwa Mungu ana jukumu la kuilinda jumuiya (taz. data 5), unabainisha pia kuwa wapo wanaoamini kuwa ni jukumu la mwanajumuiya kuilinda jumuiya (taz. kiitikio na ubeti wa 2 na 3 katika data 8 a, b na c):

(8).

**(a) Jumuiya Yetu sote tulinde**

**Tuwajibike tuimarike**

Umoja wetu ni nguzo yetu

Idumu Jumuiya yetu (kiitikio)

**(c) Viwandani na hata**

**mashambani**

**Tufanye kazi sote kwa makini**

Tujitoe kwa hali na mali

Tuijenge Jumuiya bora (ubt. 3).

**(b) Uzalendo pia mshikamano**

Viwe msingi wa Umoja wetu

Na tulinde Uhuru na Amani

Mila zetu na desturi zetu (ubt. 2)

**Chanzo:** EAC, 2017

Wimbo huu, kwa kiasi fulani, umetambulisha imani za wanajumuiya mbali na kuzingatia udhanifu pekee. Pia, tofauti na wimbo wa taifa wa Kenya, ambao umewatambulisha Wakenya kama watu wanaofanya kazi kwa bidii bila kubainisha aina za kazi wanazofanya, wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, unataja kazi mahususi za viwandani na mashambani. Unawasilisha kama kwamba kazi zinazofanyika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mbili tu; viwandani na mshambani. Wimbo huu

hauwatambulishi wafanyabiashara, wavuvi, watumishi wa umma na wanasiasa. Pia, kama ulivyo wimbo wa taifa wa Kenya, wimbo huu hauwatambulishi watu wasiokuwa na kazi, ambao utafiti wetu uliwabaini kuwa ni wengi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, kwa kuwa wimbo huo unatokana na nyimbo tatu za washindi kutoka Kenya, Tanzania na Uganda, hauna tungo zozote kutoka Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Sudani ya Kusini. Hivyo, kuutazama wimbo huu kuwa ni utambulisho wa wakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuna walakini.

### **3.1.7 Udhaifu katika Kutambulisha Tunu za Taifa**

Eneo lingine lenye udhaifu katika nyimbo teule ni utambulisho wa tunu za taifa. Wimbo wa taifa wa Tanzania umeweka mkazo katika masuala manne ambayo ni hekima, umoja, uhuru na amani. Wimbo huo unasisitiza masuala ambayo si mionganii mwa tunu za taifa. Kama anavyosema Lugeiyamu (2020), tunu za taifa la Tanzania ni utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uwajibikaji na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Ilitarajiwa kuwa tunu hizo ndizo zisisitizwe katika wimbo wa taifa. Pia, masuala yanayosisitizwa katika wimbo wa taifa wa Tanzania yalikuwapo katika wimbo wa ANC uliozaa wimbo huo. Kwa kuwa ANC kilikuwa katika harakati za kudai uhuru, ni wazi kuwa masuala yanayosisitizwa katika wimbo wake yasingekuwa utambulisho wa Watanzania huru.

Kwa upande wa Kenya, tunu za taifa zinabainishwa katika Ibara ya 10 (2) ya Katiba ya Kenya kuwa ni uzalendo, umoja, ugawanaji madaraka, utawala wa sheria na demokrasia na ushirikishwaji (NCLR, 2011). NCLR inazitaja nyingine kuwa ni utu, haki, ujumuishi, usawa, haki za binadamu, kutokuwapo ubaguzi na ulinzi wa makundi maalumu. Vilevile, tunu za taifa la Kenya zinahusisha utawala bora, uwazi, uwajibikaji na maendeleo endelevu. Kati ya tunu hizo za taifa, wimbo wa taifa wa Kenya unaonekana kusisitiza haki, amani, uhuru, umoja, uwajibikaji na maendeleo endelevu tu. Tunu zingine kama utu, ugawanaji madaraka, ulinzi wa makundi maalumu, utawala bora, uwazi na demokrasia hazitajwi.

Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunu za jumuiya ni weledi, uwajibikaji, uwazi, ushirikiano, umoja na uaminifu (Maundi na wenzake, 2002; EAC, 2017). Tunu hizo nazo hazijatambulishwa inavyostahili katika wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wimbo huo unatambulisha masuala kama vile umoja, amani, uzalendo, kuilinda jumuiya, kufanya kazi kwa bidii na mila na desturi. Hivyo, kati ya tunu za jumuiya, zinazotambulishwa ni uwajibikaji (kufanya kazi kwa bidii) na ushirikiano (umoja) tu. Tunu zingine kama vile weledi, uwazi na uaminifu hazitambulishwi.

### **3.1.8 Udhafu katika Utambulisho wa Uimbaji na Matumizi**

Udhafu wa mwisho upo katika utambulisho wa namna ya kuimba nyimbo za taifa na jumuiya na matumizi yake. Imebainika kuwa wimbo wa taifa wa Tanzania unaimbwa kutokana na nyaraka na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa serikali. Kwa mfano, unaimbwa katika shule kutokana na Waraka wa Kamishna wa Elimu wa Mwaka 1998. Hata hivyo, hakuna mwongozo mahususi unaofafanua jinsi wimbo huo unavyopaswa kuimbwa, kupigwa kwenye ala za muziki na hata katika bendi. Matumizi yake, kwa kiasi kikubwa, yametegemea mazoea, utashi wa waimbaji au wapiga ala na matamko ya viongozi. Kutokana na hilo, kumekuwa na utofauti katika uimbaji, upigaji wa ala na hata matumizi yake. Ushuhudiaji wetu ulibainisha kuwa kuna watu wanapoimba wimbo huo huweka mkono wa kulia katika moyo lakini wengine hawaweki; na wengine wanaimba wakati wamesimama kikakamavu lakini wengine hawafanyi hivyo. Vilevile, wengine wanaimba kwenye shughuli kama vile mahafali lakini wengine hawaiambi; na wengine huimba katika michezo mbalimbali ya kimataifa lakini wengine hawaiambi. Aidha, wengine huimba wakiwa na ala za muziki wakati wengine wanaimba bila ala. Kwa ujumla, uamuvi wa ama uimbwe ama usiimbwe na ama ala za muziki zitumike au zisitumike umekuwa ukitegemea utashi wa waandaaji wa shughuli husika, matamko na nyaraka mbalimbali mahususi.

Kutokana na hilo, kama wanavyoeleza wafuasi wa Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, kumekuwa na mivutano ya mara kwa mara. Said

(2020) anabainisha kuwa tarehe 6 Julai 2020, viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) walikamatwa na polisi kwa kuudharau wimbo wa taifa. Anaeleza kuwa viongozi hao nane walikamatwa kwa kuimba wimbo wa taifa wakati wa kupandisha bendera ya chama chao. Pia, CHADEMA kilishutumiwa kwa kuubadilisha wimbo wa taifa kwa kuongeza ubeti wa tatu uliokuwa na maneno “Mungu Ibariki CHADEMA” (Matandiko na Elias, 2020). Kuongezwa kwa maneno hayo, kulikosababishwa na kutokuwapo kwa mwongozo ulio wazi kwa wananchi wa kawaida kuhusu matumizi ya wimbo wa taifa, kulisababisha mivutano baina ya chama hicho na serikali.

Hali kama hiyo inaonekana kwa wimbo wa taifa wa Kenya. Ingawa wimbo huo unalindwa na sheria na Katiba ya Kenya, mwongozo wa kina kuhusu matumizi yake haupo wazi. Hakuna mwongozo wa kina unaoeleza wapi uimbwe vipi. Kwa mfano, hakuna mwongozo unaoeleza wapi uimbwe kwa Kiswahili na wapi uimbwe kwa Kiingereza au wapi upigwe kwa ala na wapi uimbwe bila ala. Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa upande wake, una mwongozo wa kina wa namna ya kuuimba na kupiga ala za muziki na masuala mengine. Hata hivyo, hauelezi wapi uimbwe na ala na wapi uimbwe bila ala. Hivyo, uimbaji na matumizi ya nyimbo za taifa na jumuiya teule havitambulishi utaifa na ujumuiya bali utashi wa waandaaji wa shughuli ambapo wimbo husika unaimbwaa. Kutokana na hilo, kama inavyofafanuliwa katika Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, nyimbo hizo zipo katika nafasi nzuri ya kusababisha migongano baina ya wanajamii na serikali. Hii ni kwa sababu wanajamii husika wamewekewa mazingira mengi ya kuona hawatambuliwi katika nyimbo hizo.

#### **4.0 Hitimisho**

Kwa ujumla, imebainika kuwa nyimbo teule zina dosari mbalimbali zinazozifanya zisiwe utambulisho wa kweli wa taifa au jumuiya husika. Kutokana na dosari hizo, kuzitazama nyimbo hizo kuwa zinatambulisha wanajamii wa taifa na jumuiya husika ni suala lenye walakini. Aidha, kutokana na nyimbo hizo kushindwa kuwatambulisha wanajamii husika,

kumekuwa na mivutano mbalimbali. Pia, kumewafanya wanajamii wengine kuziona nyimbo hizo kuwa si zao. Hivyo, wito unatolewa wa kufanyika mabadiliko katika nyimbo hizo ili kuzifanya kuwa utambulisho wa taifa na jumuiya husika, tamaduni na matamanio ya wananchi wa taifa na jumuiya hizo. Kufanya maboresho katika nyimbo hizo kutawafanya wanajamii wote kuzithamini na kuondoa mivutano ilioanza kubainika. Kufanya maboresho au mabadiliko katika nyimbo za taifa au jumuiya ili ziweze kuwa utambulisho wa taifa au jumuiya ni suala la kawaida. Namibia walifanya hivyo mwaka 1991, mwaka mmoja tu baada ya kuutumia wimbo wao wa taifa waliouchagua walipopata uhuru mwaka 1990, ambao ulikuwa unafanana na *Nkosi Sikelel' iAfrika* wa Afrika ya Kusini. Pia, kama tulivyoeleza awali, Zimbabwe pia walifanya mabadiliko ya wimbo wa taifa mwaka 1994.

## Marejeleo

- Bornman, E. (2006). National symbols and nation-building in post-apartheid South Africa. *International journal of intercultural relations*, 30:383 – 399.
- Bristow, M. J., na Reed, W. L. (Wah.). (2002). *National anthems of the world* (Juzu la 10). London: Cassell.
- Cerulo, K. (1993). Symbols and the world system: National anthems and flags. *Sociological forum*, 8(2), 243–271.
- Daily News*. (2013 Juni 27). Tanzania: Dons fault court over suspension of students. Ilipakuliwa kutoka <https://allafrica.com/stories/201306170026.html>.
- East Africa Community [EAC]. (2017). *East African community anthem*. Arusha: Mwandishi.
- Gahnström, S. C. (2012). Ethnicity, religion and politics in Tanzania (Tasinifu ya umahiri). Chuo Kikuu cha Helsinki.
- Gathogo, J. M. (2015). Ecclesiastical and political leaderships in one armpit: Reconstructing the memory of Thomas Kalume (1925-75). *Studia*

*Hist. Ecc.* 41 (3): 92- 110. <http://dx.doi.org/10.17159/2412-4265/2015/451>.

Gilboa, A., na Bodner, E. (2009). What are your thoughts when the national anthem is playing? An empirical exploration. *Psychology of music*, 37(4), 459–484.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania [JMT] (ht.). Wimbo wa taifa. Iliyopakuliwa kutoka katika Tovuti kuu ya Serikali kwenye <https://www.tanzania.go.tz/home/pages/259> tarehe 26 Machi 2022.

Jules-Rosette, B. na Coplan, D. (2004). “Nkosi sikelel’ iAfrika:” From independent spirit to political mobilization. *Cahiers d’études africaines*, 173-174: 343-367 Iliyopakuliwa kutoka <https://doi.org/10.4000/etudes.africaines.4631>.

Kapama, F. (2013 Julai 15). Students win appeal against singing national anthem. *Daily News* Uk. 3.

Kibakaya, E. (2013 Agosti 18). How much of our religion must we bring to school? *The Citizen* Uk. 4.

Kolsto, P. (2006). National symbols as signs of unity and division. *Ethnic and racial studies*, 29(4), 676–701.

Lenjima, J. (2019). Kuchunguza maana ya majina asilia ya watu katika jamii ya Wajita Mkoani Mara Nchini Tanzania (Tasnifu ya umahiri). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Lugeiyamu, F. (2020 Disemba 23). Magufuli anavyodumisha tunu za taifa. *Habari Leo* Uk. 1.

Matandiko, K. na Elias, P. (2020 Agosti 6). Chadema launches 2020 election manifesto. *The Citizen* Uk.1.

Maundi, M, Tua, T, Kilangi, A. na Imanjama, F. (2002). *Ujue mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki*. Dar es Salaam: Friedrich Ebert Stiftung.

- Mpiga Chapa wa Serikali. (2000). *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977*. Dar es Salaam: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Msanjila, Y. (2003). Kushuka kwa hadhi ya lugha za jamii Nchini Tanzania. *Nordic journal of African studies* 12(3): 296–309. Helsinki: Nordic Association of African Studies.
- Mutamererwa, S., Chamisa, V. na Chambwera, G. (2013). The national anthem: A mirror image of Zimbabwean identity? *Muziki* 10(1):52-61.
- Nairobi: National Council for Law Reporting [NCLR]. (2011). *The constitution of Kenya, 2010*. Nairobi: Mwandishi.
- Ndimandea, J. na Moyo, K. (2018). Singing the Zimbabwean nation: Nationalism, landscapes of memory and the state. *Journal of politics and good governance* IX (9.1):1-18.
- Ngaira, A. (2015 Disemba 12). The national anthem: Whose composition? Ilipakuliwa kutoka <https://nairobinews.nation.co.ke/news/the-national-anthem-whose-composition>.
- Ngure, A. (2003). *Fasihi simulizi kwa shule za sekondari*. Nairobi: Phonex.
- Nikitina, A. (2011). *Succesful public speaking*. Moscow: Bookboom.com.
- Said, K. (2020 Septemba 9). Tanzania: Freedoms threatened ahead of elections. *The Citizen* Uk. 2.
- Sanga, I. (2018). The story of Tanzania's national anthem, 'Mungu Ibariki Afrika:' The song, travels and metamorphosis. Makala iliyowasilishwa katika warsha mjini Munich tarehe 1–3 Machi 2018.

- Tajfel, H. na Turner, J. C. (1979). An integrative theory of intergroup conflict. Katika W. G. Austin, na S. Worchel (Wah.), *The social psychology of intergroup relations*. Monterey, CA: Brooks/Cole
- Tajfel, H. na Turner, J. C. (1986). The social identity theory of intergroup behavior.
- Katika Worchel, S. na Austin, W.G., (Wah.), *Psychology of intergroup relation*. Chicago: Hall.
- The Citizen* (2018a Novemba 14). EAC anthem composer yet to be paid for task of 2010. *Mwananchi* Uk. 7.
- The Citizen* (2018b Novemba 27). New twist in EAC anthem saga. *Mwananchi* Uk. 6.
- Olali, T. (2015). Trends and development of the Swahili drama since 1957 to 2014. *International journal of humanities social sciences and education*, 2 (10):1-7.
- Oluoch, L.W. (2015). The challenges facing the Eastern African Community in conflict intervention: A Study of Eastern African Standby Force (EASF) as regional security mechanism. Tasinifu ya umahiri: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Safaris, T. (2014). Pride of place: Tanzania's national anthem. Ilipakuliwa kutoka <https://thomsonsafaris.com/blog/tanzania-national-anthem/> tarehe 26 Machi 2022.
- Wakumelo, M. (2013). Cacophony in unison: Translation strategies in achieving 'singability' in the Silozi and Citonga versions of the Zambian national anthem. *Journal of studies in humanities and social sciences*, 2(2):23-38.
- Wamitila, K. (2010). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi*. Nairobi: Focus Books.
- Vambwe, M.T. na Khan, K. (2009). Reading the Zimbabwean national anthem as political biography in the context of crisis. *Journal of literary studies* 25(2):25-39.

Van Pelt, P. (1971). *Bantu customs in Mainland Tanzania*. Tabora: T.M.P Book.